

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

Simu: 026-2322129

Nukushi: 026 -2322126

Baruapepe: km@michezo.go.tz

Tovuti: www.michezo.go.tz



Mji wa Serikali- Mtumba,
Mtaa wa Michezo,
S. L. P 25,
40481 DODOMA.

TAARIFA KWA UMMA

**BARAZA LA MICHEZO LA UMOJA WA AFRIKA KANDA YA IV NGAZI YA MAWAZIRI
LAAZIMIA TANZANIA KUWA MAKAO MAKUU YA SEKRETARIETI YA BARAZA HILO**

Arusha, 04 MEI, 2023

Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Balozi Dkt. Pindi Hazara Chana anayofuraha kuwajulisha Watanzania kuwa kikao cha Baraza la Michezo la Umoja wa Afrika Kanda ya IV Ngazi ya Mawaziri kimeichagua Tanzania kuwa Makao Makuu ya Sekretarieti ya Baraza hilo.

Aidha, wajumbe wa mkutano wameazimia kuwa mkutano ujao utafanyika hapa nchini huko Zanzibar mnamo mwezi Aprili 2024 ikiwa ni mkutano wa pili wa Baraza hilo.

Hayo yote yamewezekana kutokana na utayari wa nchi yetu kuanzia Viongozi Wakuu wa nchi wakiongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kupitia salamu zake alizowasilisha wakati wa mkutano kwa njia ya mtandao kwa wajumbe wa mkutano pamoja na Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa aliyewaomba kura wajumbe hao wakati wa mkutano huo.

Pia mkutano huo umefanya marekebisho ya Katiba yake ili kuongeza ufanisi kwa kuboresha, kukuza na kuendeleza michezo miongoni mwa nchi wanachama ambazo ni Comoro, Djibout, Eritrea, Ethiopia, Kenya, Madagascar, Mauritius, Rwanda, Somalia, Sudan, Sudan Kusini, Shelisheli, Tanzania na Uganda.

Imetolewa na

Eleuteri E. Mangi

KAIMU MKUU WA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI

WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO